Toleo 17

# Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA KAZI YA KIMISHENI ULIMWENGUNI KOTE

## KUTUMA WAFANYI KAZI WALIOHITIMU

Hapo mwakani 759 Kabla ya Kristo Kuzaliwa (KK) nabii Isaya alisikia sauti ya Bwana ikimuuliza: "Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?" (Isaya 6:8). Je, ni nani atachukua Neno la Mungu na kulishiriki kwa watu ambao wanalihitaji sana? Ni nani ambaye atatoa muda na talanta zake na kuacha mambo ya dunia ili kujitoa mhanga kwa ajili ya matakwa na kazi ya Mungu? Ni nani ambaye ataacha kutilia maanani sifa zake za kibinafsi na maisha yake ya kibinafsi na kunena ujumbe wa kweli wa Mungu? Je, ni nani ambaye yuko tayari kustahimili kukataliwa na wanadamu na kudhihakiwa kwa ajili ya injili? Ni nani ambaye yuko tayari kukumbatia ukweli wa hali ya juu sana kuhusu tumaini na utakatifu wa Mungu? Nabii Isaya alisikia wito wa Roho Mtakatifu naye akatoa jibu lake: "Mimi hapa, nitume mimi" (Isaya 6:8).

Mathayo 9:37 inasema hivi: "Mavuno ni mengi, lakini wafanya kazi ni wachache." Mungu anawatafuta watu waaminifu na waliohitimu na kuojitoa kwake kama dhabihu iliyo hai madhabahuni mwake. Anawatafuta watu ambao wako tayari kutoa maisha yao kwa ajili ya kusambaza ujumbe wa milele na kupeleka wokovu katika ulimwengu wote uliopotea. Yeye ana wito maalum na mahali maalum katika mwili wa Kristo kwa kila mmoja wetu. Na ingawa kuna hitaji kubwa la wahudumu wa injili na waalimu na mishenari, kusudi kubwa la Mungu ni kwamba kila mhudumu wa injili awe amehitimu kiroho kwa ajili ya kazi hiyo.




Mungu anawatafuta wafanyi kazi walio mfano bora wa kile ambacho biblia inamaanisha inaponena kuhusu mtu kuishi maisha matakatifu na yasiyo dosari katika ulimwengu huu mwovu. Timotheo wa Pili 2:6 inasema, "Yampasa mkulima mwenye bidii ya kazi kuwa wa kwanza wa kupata fungu la mavuno." Ili kufaulu katika kazi yake mhudumu wa injili anahitaji kujua wokovu wake kwa njia ya kibinafsi, ili kwa msingi huo wa wokovu wa kibinafsi mhudumu aweze kunena kwa ujasiri na uhakika. Kabla ya kufanya kazi ya Mungu, mhudumu wa injili anahitaji kujazwa nguvu za Roho Mtakatifu (Matendo 1:8). Roho wa Mungu ndiye anayetoa mwongozo katika kazi ambayo Mungu amemwitia mhudumu wake. Roho Mtakatifu ndiye humpatia mhudumu faraja, malengo bora, mamlaka ya kiungu, na hata upako.

Mhudumu wa kweli wa Mungu anahitaji kuhudumu kwa roho ya unyenyekevu, nia yake ikiwa tayari kuwa mtumishi, awe mtu asiyeongozwa na tamaa za kupata mali, ama kiburi, ama kwa minajili ya kupata mamlaka (1 Petro 5:2-3). Anahitaji kuwa mfano bora kwa kanisa (1 Timotheo 4:12), pia awe mtu aliyehitimu katika matakwa yote yaliyowekwa katika biblia kwa ajili ya viongozi wa kanisa (wazee wa kanisa/au wahudumu wa kanisa). Hii ni kulingana na jinsi matakwa hayo yamewekwa katika 1 Timotheo 3:1-7 na Tito 1:7-9. Zaidi ya hayo, anahitaji kuwa mtu asiye na ila wala dosari maishani, mwenye tabia nzuri, mtu anayeweza kutolewa ripoti bora na watu wale wengine, mtakatifu, mwenye haki, aliye na kiasi, mwaminifu, makini, asiyeshiriki ulevi, na mwenye subira na ukarimu. Kama alishaoa anahitaji kuwa mume wa mke mmoja, na mtu mwenye kusimamia nyumba yake vizuri. Asiwe mtu mwenye

*(Inaendelea kutoka ukurasa 2)*


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Tahariri | Kujifunza Biblia: Huduma | Funzo la Kushiriki:Nalo: Huduma | Maswali na Majibu | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu |
| 3 | 4 | 5 | 7 | 8 |

# Mambo Yenye BIBLIA Inafundisha Kuhusu...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35
**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21
**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10
**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6
**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11
**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8
**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22
**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36
**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18
**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4
**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, 1 Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17
**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16
**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, 1 Kor. 7:10-11
**Urembo wa Nje**
1 Tim. 2:9-10, 1 Kor. 11:14-15, Kum. 22:5
**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46
**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20
**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17
**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Endelea kutoka ukurasa 1)*

ugomvi (2 Timotheo 2:24), mbali awe mtu anayefuata haki katika mahusiano yake na watu wale wengine (1 Timotheo 5:21), na asiwe mshiriki wa ulevi.

Mhudumu wa Mungu anahitaji kuwa na uwezo wa kufundisha (2 Timotheo 2:24), pia awe mwenye uwezo wa kufafanua imani za Kikristo na pia kufafanua maneno ya uhai (2 Wakorintho 3:5-6). Hilo ni jambo ambalo silo tu lenye umuhimu, mbali pia ni la lazima. Kama jinsi ni vigumu watu kumsikiliza mwimbaji ambaye hana uwezo wa kuimba, au wanafunzi kumsikiliza mwalimu ambaye hana uwezo wa kufundisha, ndivyo ambavyo Wakristo hawawezi kumsikiliza mhubiri ambaye hana uwezo wa kuhubiri. Wahudumu wanahitaji kumtumikia Mungu kulingana na karama waliyopewa na Mungu, na kuwa waangalifu ili wasifanye huduma hiyo bila kuzingatia karama waliopewa na Mungu.

Katika 1 Wakorintho 12:18 tunasoma kwamba, “Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka.” Wahudumu wa kweli huwa na wito wa Mungu, wao hawachaguliwi na wanadamu, na pia huduma yao haitokani na shauku zao za kibinafsi. Wao huhitimishwa na Roho, na kamwe hawahitimishwi na masomo waliyosoma.

Sauti ya Mungu ingali inaitana, Roho wa Mungu angali amtafuta mtu atakayeitikia wito wa kiungu wa kwenda ulimwenguni kote kuhubiri injili kwa kila kiumbe (Mariko 16:15). Kwa kweli hakuna wito mkuu zaidi kuliko huo, hakuna malengo makubwa maishani mwa mwanadamu kuzidi kuitikia wito wa Mungu na kufanya kazi shambani lake kwa ajili ya kuokoa nafsi za wanadamu.

—mws

## UKWELI WA INJILI

Gazeti la ‘*Ukweli wa Injili*’ huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi ktuokana na dhambi unaoletwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinafsi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

## UAGIZAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anavyotuongoza. Tutembelee katika mtandao wetu wa www.thegospeltruth.org ili uagize kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe ili upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

## WASILIANA NASI

Gazeti la *Ukweli wa injili* linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimisheni ambazo sisi hutenda huwezeshwa kupitia kwa matolea ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

---

Ukweli wa Injili, 605 Bishops Ct., Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

# Tahariri



*Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema!* –Warumi 10:14-15

Tunahitaji kumshukuru Mungu kwa sababu ya watumishi wake wa hapo mbeleni ambao walimtumikia na ambao walikuwa tayari kuweka maisha yao hatarini kwa ajili ya injili. Wao walikuwa na maono ya mbinguni, na walifanya kazi ya Mungu kwa uaminifu ili kuleta tumaini na hukumu zinazotokana na neno la Mungu. Injili ndio ukweli ambao hubadilisha maisha ya mwanadamu, na katika giza lililoko katika jamii za kisasa kungali na hitaji kubwa la kuhubiri ukweli wa Neno la Mungu. Ulimwengu wa kidini wa siku hizi umejaa manabii wa uongo, na pia umejaa wahudumu ambao wanahubiri wokovu wa kuwaletea watu furaha ya "kujihisi vizuri," wengi wao kamwe hawahubiri ujumbe ulio wa kweli, ujumbe wenye kuleta toba na utakatifu kwa mwanadamu. Lakini ukweli kamili usio na dosari ungali unazo nguvu za kuwatenganisha mwanadamu na dhambi kupitia kwa nguvu za Kristo.

Katika robo hii ya mwaka mimi nina mzigo mkubwa moyoni mwangu kwa ajili ya somo la huduma ya Kristo. Kuna haja kubwa ya kupatikana kwa wahudumu wa Mungu ambao wamehitimu na ambao wako tayari kuitikia wito wa Mungu wa kuhudumu Injili. Ukweli ni kwamba, kuna unafiki mkubwa katika ulimwengu wa kidini, na ndiposa jina la Ukristo limepata pigo kubwa. Hebu basi niwakumbushe sifa zinazomhitimisha mhudumu wa Mungu ili sote tufanye juhudi za kushikilia sifa hizo kama mwili wa Kristo. Kwa kufanya hivyo sisi wa kizazi hiki hatutaruhusu historia yetu ya pamoja, urafiki wetu, au ujamaa wetu kushusha kiwango hicho cha Biblia. Ni jambo muhimu kwa wahudumu walio uongozini kuwa watu wanyenyekevu na wao kuendelea kumtegemea Bwana wao. Ukweli ni kwamba kuna hali ya watu wote kutoshana katika Kanisa la Mungu, na ni muhimu kwamba Mungu anapoita wahudumu wake wasiwe watu wenye roho ya kujihisi kwamba wao ni (watu) muhimu sana au kujihisi kwamba wao wamekalia vyeo vikubwa.

Wahudumu wa Mungu hupitia hali ngumu maishani, lakini hakuna jambo linaloweza kuleta utoshelevu moyoni kuliko mtu kufanya kazi chini ya upako wa Roho Mtakatifu. Sisi ndio ambao tumekabidhiwa injili ya wakati wetu, na hivyo tunahitaji kupata himizo jipya mioyoni mwetu na kuinua vinywa vyetu na kupaza sauti zetu kuzifanya kuwa tarumbeta ambazo zinatoa sauti kamili ya ujumbe wa kweli. Watu walioko kanisani ndio ambao mara nyingi huwa tayari kuwaangusha wahubiri, badala ya wao kukubali ukweli kwamba hawako tayari kupokea ukweli. Basi wahudumu wa Injili wanahitaji kuwa na ujasiri unaotokana na Roho Mtakatifu na kuendelea kuhubiri Injili ya ukweli. Ujumbe ambao una dosari ndani yake utaingiza dosari ndani ya Ukristo wetu, na ujumbe wenye misimamo mikali ya kidini utazaa Wakristo wenye misimamo mikali ya kidini. Basi ni jambo muhimu wahudumu wa Kristo kutoegemea kushoto ama kulia katika mahubiri ya ukweli.

Katika jalida hili pia tutaangazia kidogo swala la kuwaamua wahudumu. Mafundisho ya kuwaamua wahudumu ni mafundisho ambayo yanalingana na mafundisho bora ya Biblia, na ni swala muhimu kwa wahudumu wa Kristo. Nalo ni jambo muhimu kwa Wakristo wote kwa jumla kuweza kulielewa. Ingawa watu wengine wanaepuka ukweli na mafundisho ya kuamua wahudumu wa injili kwa sababu hilo ni jambo linaloweza kuangazia mambo magumu maishani mwao, tunahitaji kuwa waaminifu ili mafundisho na mazoea ya ukweli wa kuwaamua wahudumu usipotee kutokana na hofu yetu ya ukweli huo. Ni jambo la baraka kubwa kwetu kutambua na kuwaamua wahudumu ambao wamekumbatia mafundisho timamu na wenye roho safi mioyoni mwao.

Michael W. Smith

Julai 2016

mengi kwa

MTANDAO

*Tutembelee kwa*

*www.thegospeltruth.org*

*ili uagize na kusoma*

*jarida letu.*



### Sifa za Biblia Zinazotakikana Maishani mwa Wahudumu wa Injili

Matendo 1:8 **Waliojazwa Roho** (Luka 24:49)

2 Timotheo 2:24 **Walio na uwezo wa Kuwafundisha Watu Wale Wengine** (1Timotheo 3:2)

2 Wakorintho 3:5-6 **Wanaoweza Kutekeleza Huduma** (Tito 1:9)

2 Timotheo 2:6 **Wanaowezaa kushiriki mavuno ya kwanza.**

1 Petro 5:2-3 **Wenye nia yenye utayari. Walio mfano bora kwa Wakristo** (1 Timotheo 4:12)

Matendo 20:19 **Wanyenyekevu**.

1 Timotheo 3:1-7 na Tito 1:7-9 **zinasema kwamba awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkarimu, ajuaye kufundisha, asiwe mtu wa kulewa, asiye dhalimu; awe mpole; asiwe mbishi, wala asiwe mwenye kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; wala asiwe mtu aliyeongoka karibuni, tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje.**

# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## SOMO: HUDUMA

**Somo la Biblia:** *Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe.* —Waefeso 4:11-12

**Muhstasari:** Wahudumu wanahitaji kuwa viongozi wa kiroho waliohitimu, wenye uwezo wa kufaulu katika huduma, na walio mfano bora kwa Wakristo. Pia wanahitaji kuhubiri injili kwa uaminifu na kuwaonya watu kulingana na ukweli na upendo, huku wakiwa na upako wa Roho Mtakatifu.

**I. Amri ya Kuhudumu**
- A. Mathayo 28:19-20 Nendeni mfundishe.
- B. Marko 16:15-16 Kuhubiri injili ulimwenguni kote.

**II. Kazi Kubwa za Wahudumu**
- A. 2 Wakorintho 5:20 Mabalozi wa Kristo
- B. 1 Wakorintho 4:1 Waliotunukiwa siri za Mungu.
- C. Wafilipi 1:7 Watetezi wa Injili

**III. Wajibu wa Wanaohudumu (Agano la Kale)**
- A. Isaya 58:1 Kutoa sauti ya kilio, bila kukoma
- B. Isaya 62:6-7 Walinzi waliosimama ukutani.
- C. Yeremia 23:1-5 Wachungaji waaminifu
- D. Ezekieli 3:17-21 Waliowajibika kwa ajili ya kutoa onyo.

**IV. Jukumu la Kuhubiri Neno**
- A. Waefeso 3:8-9 Kuhubiri utajiri wa Kristo usiopimika.
- B. Matendo 5:19-20 Kunena maneno yote kuhusu maisha haya.
- C. Matendo 20:26-31 Kutangaza hekima yote ya Mungu; Kusimamia na kulilisha kanisa, kuwa macho na kukanya.
- D. Tito 2:15 Kuonya na kukaripia kwa mamlaka yote.

**V. Jinsi ya Kuhubiri**
- A. 2 Wakorintho 4:5 Kumhubiri Yesu, sio kujihubiri.
- B. 1 Korintho 2:1-5 Sio kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, mbali kwa nguvu.
- C. 1 Peter 4:11 Kwa maneno ya Mungu na kwa ajili ya utukufu wake.
- D. Waefeso 4:15 Kunena ukweli kwa upendo.
- E. Matendo 20:20, 27 Kunena yote bila kukoma.
- F. 1 Wathesalonike 2:4-5 Asiwe mtu wa kuwapendeza wanadamu (Wagalatia 1:10-11).
- G. Mathayo 10:28 Kuhubiri bila kumwogopa mwanadamu.
- H. 2 Wakorintho 3:12 Kutumia lugha ya wazi.

**VI. Wajibu Mwingine wa Wahudumu**
- A. 1 Wathesalonike 5:14 Kuonya, kutia moyo, kutia nguvu, kuvumilia.
- B. 2 Timotheo 2:15 Kusoma, kutafakari, kujiandaa (1 Timotheo 4:14-16).
- C. Mathayo 10:7-8 Kuhubiri bila kulipisha.


**Tamati**

*Lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho . . . Bali wewe, uwe mwenye kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiza hudumu yako kwa ukamilifu* (2 Timotheo 4:2-5).

# Huduma

### Wanahitaji Kuwa Wameitwa na Mungu

Roho wa Mungu ndiye huwahitimisha na kuwaita mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu. Wahudumu wa injili huitwa kwenye huduma kwa ajili ya "kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe" (Waefeso 4:13). Yesu ndiye aliyewapatia wanafunzi wake wajibu wa kufanya, na angali awapatia wanafunzi wake kazi ya kufanya mpaka sasa, ili waweze kwenda kote ulimwenguni na kuhubiri injili (Marko 16:15-16). Ni mwito mkuu mtu kuitwa kuhudumu Neno la Mungu, kwani kazi hiyo ndiyo itakayoamua nafsi za wanadamu zitaishia wapi. 1 Timotheo 3:1 inasema kwamba "Ni neno la kuaminiwa; mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema." Hii sio kazi ya mtu kuchukulia kwa wepesi ama kwa njia ya hivi hivi tu. Huduma inahitaji kutokana na wito wa Mungu na pia inahitaji kuwa na upako wa Roho Mtakatifu.



### Wafanyi Kazi Waliohitimu

Wahudumu wa Injili huitwa ili kuwa mabalozi wa Kristo na wanahitaji kumwakilisha katika kila fani ya maisha. Mtume Paulo katika Waefeso 4:1 anawarai wahudumu "mwende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa." Wahudumu wanahitaji kuleta utukufu kwa jina la Kristo kupitia kwa roho ambaye wanamdhihirisha, mavazi yao, na hata kwa jinsi wanavyoishi. Wahudumu ambao hawajahitimu na kupata sifa za kibiblia hawastahili kuwa katika huduma mpaka sifa za maisha yao ifikie kiwango hicho na pia kuwa wameitwa na Bwana. Wahudumu wamepewa jukumu la kuwa "mawakili wa siri za Mungu" (1 Wakorintho 4:1) na kuwa walinzi na kinga ya imani.

Kazi ya Mungu kote ulimwenguni imepata kukwazika kutokana na kuweko na wahudumu wasio wa kweli, na kwa ajili ya kuweko na wahubiri wa Neno la Mungu ambao hawajahitimu. Dini imekuwa sasa ni biashara kwa wahudumu wengi. Lakini wahudumu wa kweli wa Injili ni watumishi wa watu wale wengine na wanafanya kazi hiyo sio kwa ajili ya maslahi yao binafsi mbali kwa maslahi ya watu wa Mungu: "lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana wa wale walio chini ya utunzaji wao, bali iweni mifano kwa lile kundi" (1 Petro 5:2-3). Nayo Mathayo 10:8 inasema, "Mmepata bure, toeni bure."

### Walinzi Waliosimama Ukutani

Agano la Kale linatoa mwongozo mkubwa ambao unaweza kutumiwa hata wakati wa sasa linaposema kwamba, "Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu; hawatanyamaza mchana wala usiku; ninyi wenye kumkumbusha BWANA, msiwe na kimya" (Isaya 62:6). Nayo Isaya 58:1 inasema kwamba, "Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubirie watu wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao." Mungu amewaweka wahudumu kuwa walinzi waliosimama kwenye kuta za mijengo ili wahubiri injili ya milele ambayo inaleta uhai (kwa uhai) na kifo (kwa kifo). Ikiwa mhudumu atamwona adui akifanya kazi kati ya watu wa Mungu na kukosa kupiga kelele kuwaonya, mhudumu huyo atawajibika kwa ajili ya nafsi zao zitakazopotea (Ezekieli 3:17-21). Lakini kama mhudumu wa injili atatangaza ujumbe wa Mungu lakini watu hao wapotee, yeye hatachukuliwa kuwajibika kwa ajili ya dhambi na matendo maovu ya watu hao. Basi ni jambo lenye uzito mkubwa kwa mtu kujiita mhudumu wa Inji ya Bwana kwani kazi hiyo inadai uwajibikaji wa kiwango cha hali ya juu.

### Jukumu la Kuhubiri Neno la Mungu

Wahudumu wa Kristo wameitwa ili wahubiri utajiri wa Kristo ambao haupimiki (Waefeso 3:8) na ili kuwaambia "watu maneno yote ya Uzima huu" (Matendo 5:20). Ni furaha kubwa na wadhifa mkuu kwa mwanadamu kushiriki ujumbe wa tumaini na wokovu kupitia kwa Yesu Kristo. Wahudumu wanahitaji kuwa kama mtume Paulo ambaye alinena na kusema: "Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu." Ni kweli kwamba mtu akihubiri ukweli atapata pingamizi kutoka nje na ndani ya kanisa, lakini wahudumu wa injili wanatakiwa kuwa waaminifu na


*(Inaendelea kutoka ukurasa 6)*

(Endelea kutoka ukurasa 1)

wanatakiwa ku - "onya na kukaripia kwa mamlaka yote" (Tito 2:15). Wahudumu wa Kristo hawastahili kuhubiri ili kumpendeza mwanadamu mbali kwa kumpendeza Mungu (1 Wathesalonike 2:4-5). Jumbe za injili zinahitaji kuhubiriwa bila kumwogopa mwanadamu yeyote (Mathayo 10:28) au kuhofu mateso ambayo yatamjiri mhudumu baada ya mahubiri kutolewa.

**Kulisha Kundi la Mungu**

Mungu amefanya wahudumu kuwa wasimamizi wa mambo ya kiroho na wanahitaji kutekeleza jukumu hilo wakiwa sio kama mabwana wa watu wa Mungu mbali kama watumishi na wachungaji. Kazi yao ni "kulilisha kanisa lake Mungu" chakula maalum cha kiroho. Wahudumu wanahitaji kuhubiri Neno la Mungu na kunena kulingana na mausia ya Mungu na kwa ajili ya utukufu wake (1 Petro 4:11). Wahudumu wanahitaji kuwa waangalifu sana ili wasihubiri maoni yao wenyewe, au kuhubiri tamaduni au historia za wanadamu. Wao wanahitaji kuhubiri kulingana na misingi ya Neno takatifu la Mungu ambalo halibadiliki. Wahubiri wengi hujitukuza wao wenyewe wanapohubiri na kujaribu kuwavuta watu kwao kwa njia ya kuwachekesha na kuwafurahisha wanadamu, au kwa kutumia usanifu wa lugha au maneno ya hali ya juu. Lakini mhudumu wa kweli wa Kristo anatambua kwamba Mungu "ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya" (2 Wakorintho 3:5-6), "Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu" (2 Wakorintho 4:5). Kristo anahitaji kuwekwa katikati ya kazi yote ya huduma na mwanadamu kamwe hastahili kutukuzwa katika kazi ya huduma.



**Huduma Yenye Mtazamo wa Pande Zote**

Mahubiri yaliyopakwa mafuta na ambayo chimbuko lake ni Roho Mtakatifu yanatokana na mtu kutembea na Mwokozi Yesu na pia kwa kuwa mwaminifu kutoa ujumbe wa Mungu kulingana na ulivyovuviwa na Mungu mwenyewe. Paulo alisema kwamba mahubiri yake hayakutokana na ufasaha wake wa kusema ama hekima yake ya kibinafsi. Kuhubiri kwake kuhusu Yesu Kristo "hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu" (2:4). Hata ingawa hukumu ni sehemu kamili ya huduma ya kweli yenye utakaso, msingi wa huduma yote inahitaji kuwa upendo; "Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo" (Efeso 4:15). Wahudumu wengine hukazia sana swala la hukumu hivi kwamba ujumbe wa ndani wa injili, maanake upendo, hupotea. Wengine hufanya juu chini kuwafanya wasikilizaji wao kujihisi vizuri ndiposa wanakosa kuhubiri ukweli wote ambao utamfanya mtafutaji wa ukweli kukua kiroho na kupata uhai. Basi ni jambo muhimu wahudumu kufanya huduma yao kuwa yenye mtazamo wa pande zote.

**Huduma Ambayo Inawajali Watu Wale Wengine**

Timotheo alipewa maagizo yafuatayo "ihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho" (2 Timotheo 4:2). Ni jambo muhimu kwa mhudumu kuwa mwaminifu hata ingawa atapatwa na majaribu na hisia tofauti za kibinafsi. Wahudumu wa injili wanahitaji kuwa na uvumilivu na subira nyingi na wanahitaji kumtafuta Mungu ili awape upendo wa ndani zaidi, awape pia furaha na utu wema na unyenyekevu wa Roho wa Mungu katika huduma hiyo yao. Mhudumu aliyefuzu atafanya juhudi kuwafariji na kuwaunga mkono wale wenye mahitaji na shida tofauti maishani mwao (1 Wathesalonike 5:14). Yeye anahitaji kuwa mtu mwenye subira na fadhili, akilitunza kundi la Mungu kama jinsi Yesu mchungaji mkuu anavyolichunga kanisa lake.

**Huduma Ambayo Imejiandaa Vilivyo**

Kama ilivyo kwa kazi au mwito mwingine wowote ule, wahudumu wa injili wanahitaji kujitoa mhanga kujifunza Neno la Mungu "Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli" (2 Timotheo 2:15). Kila mhudumu anahimizwa "Uyatafakari hayo; ukae katika hayo" (1 Timotheo 4:15). Pia wahudumu wanahitaji kusema "katika neno la kweli" (2 Wakorintho 6:7) na hivyo kunena hivi kwamba watu waweze kujua na kuelewa mapenzi ya Mungu kwa njia ya uwazi.

**Huduma yenye Uaminifu**

Tunaomba kwamba kila mhudumu wa Bwana awe mwaminifu kwa maono na mwito ule aliopata kutoka kwa Mungu. Neema na upendo wa Bwana Yesu Kristo, na nguvu na upako wa Roho Mtakatifu uwe juu yenu. Amina. —mws

# MASWALI na MAJIBU

**Maana ya Kumwamua Mhudumu wa Injili ni Nini?**

Kumwamua mhudumu wa injili ni kutambua wito na kuhitimu kwake kama mhudumu wa injili, kwa yeye kuwekewa mikono na wahudumu wale wengine ambao tayari washaamuriwa. Paulo alimwagiza Tito “kuwateua wazee wa kanisa katika kila mji” (Tito 1:5). “Kumwamua” inamaanisha kuchagua, kupanga, kuweka mpangilie. Paulo pia alimwambia Timotheo “uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu” (1 Timotho 1:6). Pia kunayo mifano mingine kutoka kwa Biblia ambayo inaonyesha kuwaamua wahudumu kuwa ndio uteuzi wa kiungu wa mhudumu kutambuliwa na kanisa kwa kumtenga au kumweka wakfu kwa ajili ya wajibu maalum.

Katika Matendo 13:2-4 tunasoma, “Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia. Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao. Basi watu hao, wakiisha kupelekwa na Roho Mtakatifu . . .” Basi ni dhahiri kwamba ni Roho Mtakatifu ndiye ambaye hutoa vipawa kwa wahudumu na kuwahitimisha na pia kuwatuma.

Inawabidi wahubiri na wafanyi kazi wengine wa Bwana Yesu iwe kwamba Yeye ndiye aliyewachagua na wapakwe mafuta kwa nguvu za Mungu huku wakipewa mamlaka na Yeye. Kumwamua mhudumu basi ni tendo la kibiblia ambalo linakubaliana na mafundisho ya kweli ya Ukristo, na ni tendo la kumtambua mhudumu huyo hadharini kwa kumwekea mikono huyo ambaye Roho Mtakatifu ashamchagua na kumhitimisha.

Ndugu Ostis Wilson aliandika kuhusiana na swala hilo hapo Disemba 1979 katika gazeti la *Imani na Ushindi* (Faith and Victory) na kusema yafuatayo:

Ni dhahiri kwamba kila mhudumu wa injili atajisikia kuwa yu huru zaidi kufanya huduma na kazi yake kwa njia inayofaa zaidi anapojua kwamba ametambuliwa, anaungwa mkono, na kwamba amekubaliwa na wahudumu wengine ambao wanafanya kazi pamoja, na pia kutambuliwa na Wakristo wale wengine. Ili mtu kufaulu kufanya kazi ya “Mzee wa Kanisa” ama “Askofu/msimamizi” kwa kila njia katika kusanyiko moja, anahitaji kuwa ashaamuriwa kwa kuwekewa mikono na wahudumu wengine ambao waliamuriwa hapo mbeleni. Ni kweli kwamba mhudumu anaweza kuhubiri na kulisha kundi la Bwana bila kuamuriwa, lakini kwa swala la kutumia mamlaka, ama kwa kushughulikia matatizo ambazo yanaweza kuzuka kati ya kusanyiko, yeye atafaulu zaidi na kuheshimiwa zaidi katika maamuzi yake kama atakuwa ashatambuliwa na kuungwa mkono na kanisa hilo ambalo anahudumu, na kwamba washiriki wa kanisa hilo wanamtambua kama mhudumu kamili.

**Ni nani anayestahili kuamuriwa?**

Mhudumu wa injili ambaye anatakiwa kuamuriwa anahitaji kuwa yule ambaye amehitimu katika sifa zote za biblia za msimamizi wa kanisa, na pia awe na upako wa Mungu ulio dhahiri maishani mwake na kwenye huduma yake. Anahitaji kuwa mfano bora wa utakatifu, mwenye imani timamu, na kuwa na roho kama ya Kristo maishani mwake. Mhudumu mpya hastahili kuamuriwa kwa haraka, hata kama umri na masomo yake yamemhitimisha kuamuriwa. Yeye anahitaji kupewa muda katika huduma ili kudhihirisha huduma yake katika Bwana.

Kwenye jalida la Mafundisho ya Kanisa la Mungu (Church of God Doctrines) Cecil Carver anasema kwamba “Mhudumu wa injili hastahili kuamuriwa kabla hajadhihirisha kustahili kwake. ‘Hastahili kuwa mwanagenzi,’ ni jambo linaloonyesha kwamba wahudumu wanahitaji kuwa makini sana kabla ya kumwamua mhudumu mwenzao. Lakini pia wahudumu wa injili hawastahili kuchelewa sana kumwaamua mhudumu huyo mpya.”

Kuamuriwa kwa mhudumu ni jambo nzito ambalo linastahili kushughulikiwa kwa umakini wa kiroho. Katika 1 Timotheo 5:22 Paulo alimwamuru Timotheo “Usimwekee mtu mikono kwa haraka, wala usizishiriki dhambi za watu wengine.” Kama kiongozi wa kanisa atamwamua mhudumu wa injili asiyestahili yeye atakuwa mshiriki wa kutostahili huko, kwa maana yeye ametia muhuri huduma isiyostahili. Kiongozi wa kanisa hastahili kukubali kusukumwa kumwamua mtu kama hakuna ishara ya wazi na uhakika kutoka kwake Roho Mtakatifu.

**Utaratibu Bora wa Kufuatwa Mhudumu Anapoamuriwa?**

Hata ingawa viongozi wawili au watatu wa kanisa wana haki ya biblia ya kumwamua mtu, sifa kamili ya tendo hilo la kuamua mtu linamaanisha kwamba dhehebu au kanisa hilo kwa jumla linahitaji kuunga mkono kuamuriwa kwa mtu huyu. Hii ndio maana tendo hilo la kumwamua mtu halistahili kufanywa kwa siri, mbali kwa uwazi, huku likiungwa mkono na viongozi wengine wa kanisa.

Ni wajibu wa mchungaji na wahudumu wengine wanaofanya kazi na mhudumu ambaye hajaamuriwa kupeleka jina lake kwa wazee au viongozi wa kanisa ili aweze kuamuriwa. Pia, ni jambo la busara uchunguzi ufanywe na pia maswali kuulizwa kuhusu mhudumu anayeamuriwa. Mke wake na watu wale anaowahudumia wanahitaji kupekuliwa ili kuhakikisha kwamba kuna hali ya utimamu na uhakika katika maisha ya mhudumu huyo na kwamba hakuna matatizo maishani mwake yaliyofichika. Itakuwa ni baraka kubwa kwa watu wa Mungu na pia ushuhuda wa kazi ya Roho Mtakatifu ikiwa ibada ya kumwamua mhudumu itafanyika katikati ya kusanyiko la watu wa Mungu.

Kumwamua mhudumu ni tendo la kiroho na halistahili kufanyika kutokana na msukumo wa kisiasa au kwa ajii ya kumpendeza mwanadamu. Kwa kweli hapo mbeleni kuamuriwa kwa wahudumu wa injili hakukufanyika ikizingatiwa umakinifu au kwa tendo hilo kuchukuliwa kwa uzito linalostahili. Lakini kuamuriwa kwa watumishi wa Mungu ni jambo ambalo linalingana na mafundisho bora ya biblia, na ni jambo ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya kanisa la Mungu katika siku hizi zetu. Pia ni jambo ambalo linastahili heshima. Viongozi walioamuriwa wanahitaji kupewa heshima wanayostahili kwa ajili ya kazi nzuri wanayofanya, na kwa ajili ya mamlaka yao katika Roho Mtakatifu.

—mws

JE, WAJUA?

**Takwimu kuhusu Wachungaji kwenye Ulimwengu wa Kikristo**

Asilimia 75% wanaripoti kwamba wana masumbufu mengi ya kiakili.
Asilimia 91% wameshawahi kuwa na uchovu kupita kiasi katika huduma yao, hivyo kushindwa kufanya huduma wao.
Asilimia 70% huwa na ugonjwa wa kujihisi kugandamizwa kiakili.
Asilimia 70% hawana rafiki wa karibu.
Asilimia 70% wanasema mshahara wao ni kiwango cha hali duni sana.
Asilimia 80% wanasema huduma ya uchungaji imeadhiri familia zao kwa njia isiyofaa.
Asilimia 33% wanasema kwamba huduma ni kazi ya machungu.

*(Takwimu hizi zinatoka kwa jalida la—Taasisi ya Masomo ya Uongozi ya Fuller–maanake, Fuller Institute Leadership Journal 2013, Schoeffer Institute).*

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

## Uwanadamu wa Wahudumu wa Kanisa

*Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lo lote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu* —2 Wakorintho 3:5

Ni wito mkuu kwa mtu kushiriki katika huduma ya kanisa. Wahudumu wanahitaji kuwa viongozi wa kiroho waliohitimu na ambao ni mfano bora kwa Wakristo. Nao mwili wa Kristo unahitaji kuwapa wahudumu hao heshima zao na kuheshimu wajibu ambao wamepewa na Mungu. Lakini pia ni jambo muhimu kwa watu kutambua kwamba wahudumu wa injili wangali wanadamu wa kawaida. Wahudumu sio roboti za kiroho, wao pia sio viumbe wakamilifu katika uwanadamu wao. Ukweli ni kwamba wao wanazo hisia, udhaifu, hali za kutokamilika, na hata mara nyingine wao hukosa hekima kwa maswala mengine. Pia wao hupata majaribu, hujihisi kuvunjika moyo, na hata wanaweza kujihisi kugandamizwa na masumbufu akilini mwao katika huduma. Basi ni jambo muhimu kwa watu kuelewa sifa za kazi ya huduma, na waruhusu wahudumu wao kuwa wanadamu wa kawaida, huku wakiwaonyesha upendo mkubwa na kuwajali.



Kusema kweli wahudumu wa injili hawana uwezo wa kibinafsi wa kufanya kazi ya Mungu, na pia hawana uwezo wa kufanya kazi ya Mungu kwa njia inayofaa bila kusaidiwa na nguvu na uwezo unaotokana na Roho Mtakatifu. Utoshelevu wao unatokana na Mungu. Wakati mwingi watu hutarajia cheo na ofisi ya mhudumu wa injili kuwaondolea uwanadamu wao, ambao sisi sote tunashiriki. Ni wakati ambapo mhudumu wa injili anatambua uwanadamu wake ndipo mhudumu huyo atakuwa na unyeyekevu wa kweli wa kumtegemea Bwana Wake.

Mitume na viongozi wa kiroho wa hapo mbeleni walikuwa na udhaifu maishani mwao kwa sababu wao walikuwa wanadamu wa kawaida, lakini jambo hilo halikumzuia Mungu kufanya kazi yake kupitia kwa maisha yao. Ni ombi letu kwamba kila mtoto wa Mungu na kusanyiko la Mungu litaheshimu na kutukuza viongozi wao waliojazwa Roho—huku wakitambua kwamba huduma ya Mungu hufanywa na wanadamu walio wa kawaida kabisa.

—mws

**Anwani**

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA
Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA